Tangazo la Serikali Na. 54 tarehe 20/02/2015

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA 290)

SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI ZA MWAKA, 2014.

Jina la sheria tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za(Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi za mwaka, 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Afisa muidhiniwa" Maana yake ni mtu yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kutekeleza jambo lolote chini ya Sheria Ndogo hizi,

"Halmashauri" Maana ni Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

"Kibali cha ujenzi" Maana yake ni kibali cha ujenzi kinachotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria na kanuni zake au chini ya Sheria Ndogo au kanuni zinazofanyia Mabadiliko kanuni hizo.

"Maeneo ya kata" Ina maana ya maeneo yote ya kata zinazounda mji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi pamoja maeneo yanayoainishwa kwamba ni maeneno ya

viwanda katika ramani ya mpango kabambe wa uendelezaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi.

Muda wa kulipa

"Maeneo Mengine" ni maeneo yote katika Wilaya Misungwi ambayo si maeneo ya kati.

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa.

Madaraka ya Mkurugenzi

4.-(i) Halmashauri itatoza ada na Ushuru Ulioorodheshwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi kwa ajili ya kupata huduma, vibali na leseni zinazotolewa na Halmshauri.

Ilani

(ii) Ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi unapaswa kulipwa kabla ya mlipaji kupata huduma inayolipiwa na kwa vyovyote vile haitazidi tarehe 30 ya mwezi wa June ya mwaka unaolipwa.

Makosa na Adhabu

5 Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na madaraka ya kufifisha kosa kwa kumtaka mtu aliyekiri kufanya kosa chini ya sheria Ndogo hizi kulipa kiasi cha fedha kisichozidi kiwango cha juu cha faini kilichowekwa chini ya sheria Ndogo hizi.

Tangazo la Serikali Na. GN/198/2001.

6.-(i) Mtu yeyote ambaye atashindwa kutekeleza maagizo yoyote yatakayotolewa kwa ilani na Halmashauri chini ya Sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

(ii) Bila kujali masharti yaliyomo kwenye aya ndogo (i) ya sheria Ndogo hii ni kosa kwa mtu yeyote kutotii ilani iliyotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa sheria ndogo hizi.

7. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatiikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu(300,000) au kifungo kisichozidi miezi 12 au vyote kifungo na faini kwa pamoja.

8. Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya Misungwi (Misungwi District Council) (Ferry Fees) by laws 2001 zinafutwa.

# JEDWALI

| **AINA YA ADA AU USHURU** | **KIWANGO CHA ADA AU USHURU** |
|---|---|
| **SEHEMU YAKWANZA** | |
| **Ada kwa kukodi au kupanga Majengo ya Halmashauri (Siyo nyumba za Wafanyakazi)** | |
| 1. Nyumba za kuishi | 1. Asilimia 15 ya thamani ya nyumba ya kuishi kwa mwaka. |
| 2. Nyumba ya biashara | 2. Asilimia 20 ya thamani ya nyumba ya biashara kwa mwaka. |
| 3. Mikataba | 3. Kiasi ambacho kimeainishwa katika mkataba husika lakini kisipungue viwango vilivyoonyeshwa sehemu 1 na 2 hapo juu. |
| 4. Kumbi za Halmashauri | 4. Ukumbi mkubwa 250,000/= kwa siku |
| | Ukumbi mdogo 150,000/= kwa siku. |
| 5. Kodi ya pango ya vibanda vya sokoni na vile vya Stendi ya Halmashauri | 5. shilingi 60,000/= kwa mwezi |
| **SHERIA YA PILI** | |
| 1.Ada ya kupima wahudumu wa nyumba ya kulala wageni, Hotel, Mgahawa, Muuzaji wa vyakula vilivyopikwa au kukaangwa anawajibika kusajili kwa Halmashauri ili kubainisha ukamilishaji wa afya yake kuendelesha shughuli hiyo. | 1. Shilingi 10,000/= kwa kila mtu kwa miezi 6 |
| **SEHEMU YA TATU** | |
| **Ada ya unyonyaji Maji machafu katika vyoo kwa magari ya Halmashauri** | |
| 1. Maeneo ya biashara | 1. Shilingi 55,000/= kwa kila safari moja |
| 2. Maeneo ya makazi | 2. Shilingi 30,000/= kwa kila safari moja |
| **SEHEMU YA NNE** | |
| Ada ya Mabadiliko ya Ardhi kama ifuatavyo | |
| 1. Makazi kuwa biashara | 1. Shilingi 50,000/= |
| 2. Makazi kuwa kiwanda | 2. Shilingi 100,000/= |
| 3. Makazi kuwa Housing estate (biashara n.k. | 3. Shilingi 50,000/= |
| 4. Viwanda/Biashara kuwa kituo cha mafuta. | 4. Shilingi 150,000/= |
| 5. Kugawanya viwanja au shamba | 5. Shilingi 150,000/= |
| 6. Kuhakiki milki | 6. Shilingi 20,000/= kwa kiwanja |
| **SEHEMU YA TANO** | |
| 1. Kibali cha kuweka konteina la biashara eneo la wazi. | 1. Shilingi 100,000/= kwa mwaka kwa kila kontena |
| 2. Kibali cha kuweka kiosks eneo la wazi. | 2. Shilingi 50,000/= kwa kila mwaka kwa kila kiosks. |
| 3. Fomu ya maombi ya biashara (Kuweka kontena kufungua kioski n.k eneo la wazi) | 3. Shilingi 15,000/= kwa kila ombi. |

**Vibali vinavyotolewa kwa biashara zifuatazo. ( Ada/Ushuru).**

| | Maeneo ya kati | Maeneo mengine. |
|---|---|---|
| 1. Magenge ya chakula (Baba/Mamalishe) | Shilingi 50,000/= kwa kila mwaka | Shilingi 30,000/= kwa kila mwaka |
| 2. Kuuza maziwa, Ice Cream, Ice Cone, Soda Juice na bidhaa Ndogo ndogo kwenye kibanda. | Shilingi 100,000/= kwa kila mwaka | Shilingi 50,000/= kwa kila mwaka. |
| 3. Kuchoma mishikaki kukaanga kuku, Supu, Chips n.k. kwenye kibanda. | Shilingi 100,000/= kwa kila mwaka | Shilingi 50,000/= kwa kila Mwaka. |
| 4. Kutengeneza viatu vipya kwenye kibanda | Shilingi 50,000/= kwa mwaka | 30,000/= kwa kila mwaka. |
| 5. Ushonaji wa nguo kwenye kibanda | Shilingi 50,000/= kwa kila mwaka. | Tshs 30,000/= kwa kila mwaka |
| 6. Fundi Radio, Luninga n.k. kwenye kibanda. | Shilingi 100,000/= kwa kila mwaka. | 70,000/= kwa kila mwaka |
| 7. Kutengeneza kuuza samani kwenye kibanda. | Tshs 100,000/= kwa kila mwaka | 70,000/= kwa kila mwaka |
| 8. Kuuza batiki vikoi n.k. kwenye vibanda. | Tshs 100,000/= kwa kila mwaka | 60,000/= kwa kila mwaka |
| 9. Kinyozi katika kibanda | Tshs 50,000/= kwa kila mwaka | 30,000/= kwa kila mwaka |
| 9. Kusuka Nywele kwenye kibanda | Tshs 50,000/= kwa kila mwaka | 30,000/= kwa kila mwaka |
| 10. Mkodishaji wa mikokoteni baisikeli kwenye kibanda/sehemu maalum | Tshs 100,000/= kwa kila mwaka | 50,000/= kwa kila mwaka |
| 12. Vikundi vya Uchukuzi na upakuaji mzigo n.k. | Tshs 100,000/= kwa kila mwaka | 50,000/= kwa kila mwaka |
| 13. Kuuza oil n.k kwenye kibanda | Tshs 50,000/= kwa kila mwaka | 40,000/= kwa kila mwaka |
| 14. Kutengeneza na kuuza mapambo ya nyumba kwenye kibanda | Tshs 55,000/= kwa kila mwaka | 30,000/= kwa kila mwaka |
| 15. Kuuza mitumba kwenye kibanda | Tshs 55,000/= kwa kila mwaka | 40,000/= kwa kila mwaka |
| 16.Biashara nyingine yoyote ndogo ndogo inayokubarika kisheria na haijatajwa katika sheria hii. | Tshs. 50,000/= hadi 100,000/= kwa kila mwaka kutegemea na ukubwa wa biashara. | 30,000/= hadi 70,000/= kwa kila mwaka. |
| **SEHEMU YA SITA** | | |
| 1. Ushuru wa mnada wa jumla | Kitu chochote kitakachonadiwa kitalipiwa ushuru kiasi cha 5% ya bei ya mnada | |
| **SEHEMU YA SABA** | | |

| | | |
|---|---|---|
| **Ada yakuzingira na kuweka majukwaa katika maeneo ya kati na maeneo mengine (ujenzi, Mikutano n.k).** | | |
| 1.Kwa mda chini ya wiki mbili | Maeneo ya kati | Menginepo |
| | Tshs. 1000/= kwa mita | Tsh. 700/= kwa kila mita |
| 2. Kwa muda chini ya wiki mbili na usiozidi wiki nne. | Shs. 2000/= kwa mita | 1500/= kwa kila mita |
| 3. Muda zaidi ya wiki 4 na usiozidi wiki 9 | Tshs. 4000/= kwa kila mita | Tshs 3000/= kwa kila mita |
| 4. Kati ya wiki 9 na usiozidi wiki 12 | Tshs. 6000/= kwa kila mita | Tshs 4000/= kwa kila mita |
| 5. Kati ya wiki 12 na usiozidi mwaka 1 | Tshs. 10,000/= kwa kila mita | Tshs 8000/= kwa kila mita |
| 6. Zaidi ya mwaka 1 | Tshs. 15,000/= kwa kila mita | Tshs 10,000/= kwa kila mita |
| **SEHEMU YA NANE** | | |
| Ada ya Nyara za Serikali | | |
| Ada ya fomu ya maombi ya nyara za Serikali | Tshs. 50,000/= | |
| **SEHEMU YA TISA** | | |
| 1. Ada ya usajili wa uchimbaji madini | | |
| (a) Usajili wa Umiliki wa madini ya ujenzi (Mchanga, kifusi n.k).<br>(b) Usajili wa umiliki wa madini ya kokoto, Moramu na chokaa | Tshs.100,000/=<br>Tshs. 150,000/= | |
| Ada ya Usafirishaji madini ya ujenzi kwa uzito | | |
| (a) Tani 1 hadi tani 7 | 5000/= kwa kila Trip | |
| (b) Tani 7 - 10 | 10,000/= kwa kila trip | |
| (c ) Tani zaidi 10 | 15,000/= kwa Trip. | |
| **SEHEMU YA KUMI** | | |
| 1. Ada matangazo ya biashara (Promotion) | | |
| (a) Utangatangazaji wa kibiashara (Business Promotion) (Internal Oriented) | Tshs. 50,000/= kwa kila Tangazo. | |
| (b) Biashara ya nje (External Oriented) | Dola za Kimarekani 70 ($ 70) kwa kila tangazo. | |

## ADA YA KIBALI CHA UJENZI

| | **Maeneo ya kati** | | | **Maneno Mengineyo** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ujazo wa juu SHS | Ujazo wa kati SHS | Ujazo wa chini SHS | Ujazo wa chini SHS | Ujazo wa kati SHS | Ujazo wa juu SHS |
| Hadi futi 500 za mraba | 30,000/= | 40,000/= | 50,000/= | 40,000/= | 30,000/= | 20,000/= |
| Hadi futi 500 hadi | 40,000/= | 50,000/= | 60,000/= | 50,000/= | 30,000/= | 20,000/= |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1000 za mraba | | | | | | |
| Hadi futi 500 hadi 1500 za mraba | 60,000/= | 80,000/= | 100,000/= | 80,000/= | 60,000/= | 40,000/= |
| Zaidi ya futi 1500 hadi 3000 | 80,000/= | 100,000/= | 120,000/= | 100,000/= | 80,000/= | 60,000/= |
| Futi 3000 hadi 4000 | 150,000/= | 200,000/= | 250,000/= | 200,000/= | 150,000/= | 100,000/= |
| Futi 4000 hadi 5000 za mraba | 170,000/= | 250,000/= | 300,000/= | 250,000/= | 170,000/= | 120,000/= |
| Futi 5000 hadi 6000 za mraba | 190,000/= | 265,000/= | 320,000/= | 260,000/= | 190,000/= | 150,000/= |
| Futi 6000 hadi 7000 za mraba | 200,000/= | 280,000/= | 350,000/= | 280,000/= | 200,000/= | 180,000/= |
| Futi 7000 hadi 10,000 za mraba | 300,000/= | 350,000/= | 420,000/= | 350,000/= | 300,000/= | 200,000/= |

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**

| | |
|---|---|
| Ada ya maengesho ya magari | |
| 1. Maegesho maalum kwa ajili ya kuegesha magari | 4000/= kwa siku au 100000/= kwa mwezi. |
| 2. Maegesho ya Umma | Tshs 500/= kwa gari kwa saa |

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**

| | |
|---|---|
| Ada ya matangazo ya biashara yaliyosimikwa kuchorwa kuchapishwa na kubandikwa katika eneo lolote la Halmashauri. | |
| 1. Yasiyowaka taa (Non – ilamunated) | Tshs 6000/= kwa futi 1 ya mraba kwa mwaka |
| 2. Yenye mwanga (illuminated advertisement) | Tshs. 8000/= kwa futi 1 ya mraba kwa mwaka na ongezeko la 3000/= kwa kila tangazo linalotokea kwa matangazo yenye kubadilika badilika. |

**SEHEMU YA KUMI NA TATU**

| | |
|---|---|
| 1. Ada ya uchinjaji | Tshs. 5000 kwa kila ng’ombe na 2000/= nguruwe na mbuzi. |
| 2. Ada ya Ukaguzi wa nyama | Tshs. 2000 kila ng’ombe<br>Tshs. 1500 kila nguruwe<br>Tshs. 1500 kila mbuzi<br>Tshs. 200 kila kuku |

**SEHEMU YA KUMI NA NNE**

| |
|---|
| **Ushuru wa uzoaji taka kwa mwezi** |

*Tangazo la Serikali Na. 54 (linaendelea)*

| Na. | JINA | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Makazi kwa kila kaya | 2000/= |
| 2. | Bihashara, Viwanda, Mashirika n.k | 50,000/= |
| 3. | Mgahawa (Tea Room) | 5000/= |
| 4. | Mgahawa (Cafeteria) -Ndogo | 5,000/= |
| 5. | Kibanda cha vinywaji baridi | 10,000/= |
| 6. | Mgahawa mkubwa | 10,000/= |
| 7. | Nyumba ya kulala wageni | 10,000/= |
| 8. | Zahanati | 10,000/= |
| 9. | Kituo cha Afya | 10,000/= |
| 10. | Hospitali | 30,000/= |
| 11. | Kiwanda cha mbao (kwa trip)<br>4.5 $M^3$<br>6.0 $M^3$<br>10.0 $M^3$ | <br>25,000/=<br>30,000/=<br>35,000/= |
| 12. | Watengeneza samani (furniture) | 20,000/= |
| 13. | Mageti na madirisha ya chuma (Karakana) | 20,000/= |
| 14. | Taka za kiwanda (Taka laini)<br>4.5 $M^3$<br>6.0 $M^3$<br>10.0 $M^3$ | <br>25,000/=<br>30,000/=<br>35,000/= |
| 15. | Kiwanda (taka ngumu) Kila tani | 10,000/= |
| 16. | Maduka ya jumla | 10,000/= |
| 17. | Maduka ya rejareja (Vyakula) | 5,000/= |
| 18. | Maduka ya rejareja yasiyo ya Vyakula | 10,000/= |
| 19. | Shule ya msingi ya kutwa ya binafsi | 10,000/= |
| 20. | Shule ya kulala ya binafsi | 25,000/= |
| 21. | Taasisi zingine za Elimu | 25,000/= |
| 22. | Grosary (Duka la Pombe) | 10,000/= |
| 23. | Baa | 15,000/= |
| 24. | Bucha ya nyama | 5,000/= |
| 25. | Duka la Dawa (Pharmacy) | 10,000/= |
| 26. | Duka la Dawa muhimu | 5,000/= |
| 27. | Soko (Kwa trip)<br>4.5 $M^3$<br>6.0 $M^3$<br>10.0 $M^3$ | <br>25,000/=<br>30,000/=<br>35,000/= |
| 28. | Shule ya msingi ya kulala ya mtu binafsi | 15,000/= |
| 29. | Shule ya binafsi ya kutwa | 15,000/= |
| 30. | Masoko ya mitaani (magenge) kwa meza kwa mwezi | 4,000/= |
| 31. | Mama lishe /Baba lishe | 4,000/= |
| 32. | Magari mazao sehemu zisizoruhusiwa (Pakua) | 10,000/= |
| 33. | Magari yanayopakua mazao sokoni $2m^3$ – $6M^3$ | 5,000/= |
| 34. | Stendi ya mabasi kwa kila basi kwa kutwa | 1000/= |
| 35. | Msikiti/Kanisa (kwa mwezi) | 5000/= |
| 36. | Biashara Ndogo ndogo | 5000/= |
| 37. | Madobi wa mitaani | 5000/= |
| 38. | Mafundi chelehani/nguo wa mitaani. | 5000/= |
| 39. | Mafundi selemala wa mitaani | 5000/= |
| 40. | Wang'arisha viatu (shoe shiners) | 5000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 41. | Mafundi simu, redio, Tv. n.k. wa mitaani | 5000/= |
| 42. | Vinyozi wa mitaani (wasio lasimu) | 5000/= |
| 43. | Kituo cha mafuta Petrili | 50,000/= |
| 44. | Kituo cha mafuta ya taa | 10,000/= |
| 45. | Ghala (ware house) | 50,000/= |
| 46. | Stoo ya mkaa | 10,000/= |
| 47. | Heoteli<br>Vyumba – 1 hadi 10<br>Vyumba 10 -20<br>Vyumba 20 – 30<br>Zaidi ya vyumba 30 | <br>25,000/=<br>30,000/=<br>40,000/=<br>50,000/= |
| 48. | Maofisi ya kazi<br>Wafanyakazi 1-10<br>Wafanyakazi 10 -30<br>Wafanyakazi 30-50<br>Wafanyakazi 50 na zaidi | <br>10,000/=<br>20,000/=<br>30,000/=<br>50,000/= |
| 49. | Lundo la taka kwa mwezi | 30,000/= |
| 50. | Taka sehemu ya ujenzi (kwa trip) | 25,000/= |
| 51. | Garage | 10,000/= |
| 52 | Car warsh | 10,000/= |

**SEHEMU YA KUMI NA TANO**

| **Ushuru wa Huduma mbalimbali** | | |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru kwa kila nyumba ya kulala wageni | Shilingi 50,000/= kwa kila nyumba kwa mwaka |
| 2. | Ushuru wa mavuno mazao mali ghafi n.k (Produce Cess) | Asilmia 5 ya thamani ya mavuno |

**SEHEMU YA KUMI NA SITA**

| **Ushuru wa mazao yatokayo nje ya Wilaya au sokoni yaliyoamuliwa** | | |
|---|---|---|
| 1. | Kuku (Kila kuku) | Tshs. 500/= |
| 2. | Nyanya tenga 1 | Tshs. 2000/= |
| 3. | Vitunguu tenga 1 | Tshs. 2000/= |
| 4. | Mchele kila gunia | Tshs. 5000/= |
| 5. | Matunda mbalimbali kwa kila tenga 1 | Tshs. 2000/= hadi 5000/= |

**SEHEMU YA KUMI NA SABA**

| **Ushuru wa stendi kwa siku** | | |
|---|---|---|
| 1. | Mabasi makubwa | Tshs. 2000/= |
| 2. | Mabasi madogo | Tshs. 1000/= |

**SEHEMU YA KUMI NANE**

| **Ushuru wa Maegesho ya Taxi na boda boda na piki piki za matailí 3 kwa mwezi.** | | |
|---|---|---|
| 1. | Taxi | Tshs. 30,000/= |
| 2. | Piki piki za tairi 3, Bajaji | Tshs. 30,000/= |
| 3. | Bodaboda | Tshs. 20,000/= |

**SEHEMU YA KUMI NA TISA**

| **Ada ya usajili kila mwaka kwa vyombo vya usafiri (Biashara)** | | |
|---|---|---|
| 1. | Taxi | Tshs.100,00/= |
| 2. | Piki piki za tairi 2, | Tshs. 50,000/= |
| 3. | Piki piki taili 3, | Tshs. 60,000/= |
| 4. | Fomu ya kusajili | Tshs.10,000/= |

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Baraza la Madiwani lililofanyika tarehe 05 mwezi Februari, 2014 na ulibandikwa mbele ya:-

NATHAN MSHANA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Wilaya ya Misungwi*

KHALID MBILIYAZA
*Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Wilaya ya Misungwi*

**NAKUBALI**

11 DESEMBA, 2014

MHE. MIZENGO P. PINDA,
*Waziri Mkuu*